JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



# MWONGOZO WA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA VITUO VYA UTAMBUZI NA UPIMAJI WA KUBAINI MAHITAJI MAALUMU YA UJIFUNZAJI KWA WATOTO NGAZI YA HALMASHAURI (ESRAC)

Oktoba, 2022

Mwongozo huu umeandaliwa na:

**OFISI YA RAIS**

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa



# DIBAJI

Ofisi ya Rais-TAMISEMI ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa utoaji wa Elimu nchini katika mazingira Jumuishi. Pamoja na usimamizi huo, ina jukumu la kusimamia ubainishaji na upimaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kabla ya kuandikishwa shule. Sambamba na hilo, inatekeleza kwa ufanisi lengo Namba 2 la Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi (2022 – 2026) linalotaka utekelezaji wa uanzishwaji wa vituo vya upimaji. Vilevile, ina jukumu la kuhakikisha kuwa wanafunzi waliobainika kuwa na mahitaji maalumu wanapewa afua stahiki kulingana na mahitaji yao ikiwa ni pamoja na kupangwa katika shule stahiki.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeona umuhimu wa kuwa na Mwongozo wenye kutambua uanzishwaji wa vituo hivyo katika ngazi ya halmashauri ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa walengwa. Mwongozo huu unatoa mwelekeo kwa halmashauri husika kutekeleza zoezi la ubainishaji na upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto kabla ya kuandikishwa shule.

Ili kufanikisha azma ya Serikali ya kutoa elimu kwa makundi yote, naelekeza Mamlaka zote za utekelezaji wa Mwongozo huu kuhakikisha zinaanzisha vituo vya upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya ujifunzaji kwa lengo la kutoa afua stahiki kwa walengwa.

Prof. Riziki S. Shemdoe
**Katibu Mkuu- Ofisi ya Rais TAMISEMI**




# SHUKURANI

Mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto ngazi ya halmashauri umeandaliwa kwa kuhusisha wataalamu kutoka OR-TAMISEMI, Taasisi za Elimu, na Wadau wa Elimu maalumu/jumuishi nchini.

Shukrani za pekee zimwendee Ndugu Geni J. Migeha (Mkurugenzi Msaidizi Elimu Maalumu, Elimu ya Watu Wazima, Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu kwa Michezo) kwa kusimamia kazi hii, Mwenyekiti wa jopo Dkt. Ildephonce Mkama (Mhadhiri – AMUCTA na Mshauri Mtaalamu wa Elimu Jumuishi – Leonard Cheshire, TO51), Mratibu wa uandaaji wa Mwongozo Ndugu Anna J. Mark (Afisa OR-TAMISEMI), Ndugu Benjamin L. Kihwele (Sense International, TO51), Ndugu Lugarata Ng'weshemi, (Afisa OR-TAMISEMI), Ndugu Mary Batamula (Kitua cha Taifa cha Upimaji – Dar es salaam), Ndugu Joachim Tamba (Mstaafu – WyEST), Dkt. Mary Runo (AMUCTA), Ndugu Fraterinus O. Mutatembwa (AMUCTA), Ndugu Upendo Komba (UDOM), Ndugu Ibrahim Suleiman (Shule ya Msingi Furaha – Tabora) na Titus J. Nyange (Light for the World).

Mwisho, shukrani ziende kwa Ndugu Ephraim A. Simbeye (Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu), Ndugu Hadija A. Mcheka (Mkurugenzi Msaidizi Elimu Sekondari), Ndugu Sussan S. Nusu (Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Awali na Msingi), ambao waliratibu na kusimamia shughuli za jopo la wataalamu katika kuandaa kitabu hiki kuanzia hatua ya awali hadi kukamilika kwake. Ni matarajio ya serikali kuwa Mwongozo huu utakuwa ni mwanzo mpya wa utekelezaji wa Elimu Jumuishi kwa ufanisi nchini.

Dkt Charles E.Msonde

**Naibu Katibu Mkuu Elimu – Ofisi ya Rais TAMISEMI**

# YALIYOMO

**DIBAJI** ..... i

**SHUKURANI** ..... ii

**MAUDHUI YA MWONGOZO** ..... 1

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Usuli ..... 1

1.3 Umuhimu wa Mwongozo ..... 2

1.4 Lengo la Mwongozo ..... 2

1.5 Matarajio ya Mwongozo ..... 2

1.6 Hitimisho ..... 2

**SURA YA PILI**

**UBAINISHAJI NA UTAMBUZI WA AWALI** ..... 3

2.1 Utangulizi ..... 3

2.2 Dhana ya ubainishaji/utambuzi wa awali ..... 3

2.3 Maeneo yanayotumika katika Ubainishaji na Utambuzi wa awali ..... 3

2.4 Viashiria ..... 3

2.4.1 Changamoto za uoni ..... 4

2.4.2 Changamoto za usikivu ..... 4

2.4.3 Changamoto za Uziwikutoona ..... 5

2.4.4 Changamoto za ufahamu ..... 5

2.4.5 Changamoto ya Ualbino ..... 6

2.4.6 Changamoto za kiafya ..... 6

2.4.7 Changamoto za kijamii ..... 6

2.4.8 Changamoto za ujongeaji ..... 6

2.5 Umuhimu wa Ubainishaji na Utambuzi ..... 7

2.6 Utekelezaji wa shughuli ya ubainishaji na utambuzi wa awali ..... 7

2.6.1 Halmashauri ..... 7

2.6.2 Wabainishaji ..... 8

2.6.3 Hitimisho ..... 8

**SURA YA TATU**

**UPIMAJI WA KUBAINI MAHITAJI YA UJIFUNZAJI** ........ 9
- 3.1 Utangulizi ........ 9
- 3.2 Dhana ya upimaji ........ 9
- 3.3 Timu ya upimaji ........ 9
- 3.4 Uanzishaji na usimamizi wa vituo vya upimaji ........ 10
- 3.5 Kanuni za uendeshaji wa vituo vya upimaji ........ 10
- 3.6 Hitimisho ........ 11

**SURA YA NNE**

**USHIRIKI WA WADAU KATIKA UBAINISHAJI, UTAMBUZI NA UPIMAJI** ........ 12
- 4.1 Utangulizi ........ 12
- 4.2 Makundi ya wadau ........ 12
- 4.3 Hitimisho ........ 13

**SURA YA TANO**

**UKUSANYAJI, UTUNZAJI NA UTUMIAJI WA TAARIFA** ........ 14
- 5.1 Utangulizi ........ 14
- 5.2 Ukusanyaji wa taarifa za upimaji ........ 14
- 5.3 Utunzaji wa taarifa za upimaji ........ 14
- 5.4 Utumiaji wa taarifa za upimaji ........ 14
- 5.5 Hitimisho ........ 15

**SURA YA SITA**

**MAJUMUISHO** ........ 16
- 6.1 Utangulizi ........ 16
- 6.2 Majumuisho ........ 16
- 6.3 Hitimisho ........ 16

**REJEA** ........ 17

SURA YA KWANZA

# MAUDHUI YA MWONGOZO

## 1.1 Utangulizi

Serikali na wadau mbalimbali wamekua wakishirikiana katika kufanya kazi za ubainishaji, utambuzi na upimaji wa watoto ili kubaini mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki. Katika usimamizi na utekelezaji wa jukumu hili, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imebaini kuwepo kwa watoto shuleni ambao hawakufanyiwa upimaji kutokana na uhaba wa vituo vya upimaji.

Hivyo, kwa kuzingatia nia ya Serikali ya kutoa elimu bora kwa wote, OR-TAMISEMI imeona umuhimu wa kuanzisha vituo vya upimaji katika ngazi ya halmashauri kwa lengo la kuwezesha kila mtoto mwenye viashiria vya kuwa na mahitaji maalumu kupata huduma ya upimaji ili kubaini mahitaji ya ujifunzaji. Sura hii inatoa mwelekeo wa uanzishwaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji katika ngazi ya halmashauri. Hivyo, inaeleza usuli, malengo na matarajio ya uanzishwaji wa vituo hivyo.

## 1.2 Usuli

Mkakati wa Utekelezaji wa Elimu Jumuishi nchini wa mwaka 2009-2017 uliainisha umuhimu wa kuwa na vituo vya upimaji kwa lengo la kubaini mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto. Katika kutekezela Mkakati huo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliandaa Mwongozo unaojulikana kama *Guidelines for Educational Support, Resource and Assessment Services* 2013 ili kuratibu uendeshaji wa vituo vya upimaji vinavyojulikana kama *Educational Support, Resource and Assessment Centers (ESRACs)*. Pia, Mkakati ulipendekeza utumiaji wa shule maalumu kama vituo vya upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu. Katika kutekeleza maelekezo ya Mkakati huo, vituo hivi vilianzishwa ngazi ya Taifa (katika kiwanda cha uchapaji wa vitabu vya maandishi ya Braille kilichopo katika shule ya Uhuru Mchanganyiko Dar es Salaam) na kwa ngazi ya Mikoa. Mkakati wa Utekelezaji wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2022-2026 umesisitiza kwamba vituo vya upimaji katika ngazi ya Taifa na Mikoa viongezwe na kuimarishwa ili kuweza kutoa huduma stahiki kwa walengwa.

OR-TAMISEMI imebaini uwepo wa changamoto ya uendeshaji wa vituo katika ngazi ya Taifa na Mikoa hali inayosababisha

watoto wenye mahitaji maalumu wanaotakiwa kupewa huduma, kushindwa kuhudumiwa ipasavyo kutokana na gharama na umbali wa kuvifikia vituo hivyo na gharama za uendeshaji. Hali hii imesababisha kuandaliwa kwa Mwongozo huu unaoelekeza uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji wa mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto kwa kila halmashauri ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa walengwa na usimamizi mzuri wa vituo.

### 1.3 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu wa upimaji wa mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto unalenga kumuwezesha Mkurugenzi wa Halmashauri katika uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji. Aidha, Mwongozo utasaidia namna ya kuboresha utoaji wa huduma stahiki za kielimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu katika ngazi ya halmashauri.

### 1.4 Lengo la Mwongozo

Lengo la mwongozo huu ni kutoa maelekezo ya uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji wa watoto ili kubainisha mahitaji maalumu ya kielimu katika kila halmashauri.

### 1.5 Matarajio ya Mwongozo

i. Kuanzishwa kwa kituo cha upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto
ii. Kuwepo kwa timu ya wataalamu wa upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto
iii. Kuwepo kwa vifaa vitakavyotumika katika kituo cha upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu kwa watoto
iv. Kufanyika kwa kazi za ubainishaji, utambuzi, upimaji na utoaji wa afua stahiki kwa wakati

### 1.6 Hitimisho

Utekelezaji wa mwongozo huu utawezesha uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji katika ngazi ya halmashauri hali itakayosaidia watoto wenye mahitaji maalumu kubainishwa na kupatiwa afua stahiki. Hivyo, Mkurugenzi wa halmashauri ahakikishe vituo hivi vinaanzishwa na vinafanya kazi iliyokusudiwa kwa ufanisi.

SURA YA PILI

# UBAINISHAJI NA UTAMBUZI WA AWALI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza kuhusu ubainishaji na utambuzi wa watoto wenye mahitaji maalumu ambapo kuna vipengele sita (6) ambavyo ni pamoja na dhana ya ubainishaji na utambuzi, maeneo yatakayotumika, viashiria vya uwepo wa mahitaji maalumu, zana, umuhimu wa ubainishaji na utambuzi, na hatua stahiki zitakazochukuliwa baada ya ubainishaji na utambuzi.

## 2.2 Dhana ya ubainishaji/utambuzi wa awali

Ubainishaji ni hatua ya awali ya uchunguzi inayosaidia kutambua kama mtoto ana au hana viashiria vya mahitaji maalumu. Katika mchakato huu ubainishaji hufanyika kwa kuangalia viashiria vya uwepo wa changamoto mbalimbali za ukuaji, uchangamano au ujifunzaji wa mtoto kutegemea mazingira yake. Ili utambuzi wa awali ufanyike na uweze kubainisha watoto wenye mahitaji maalumu, uwepo wa wataalamu na vifaa vya utambuzi ni muhimu.

Katika muktadha wa kuwatambua watoto wenye mahitaji maalumu, maneno ubainishaji na utambuzi yanatumika kwa pamoja yakimaanisha kuwa ni mchakato wa kubaini  viashiria vya hali ya kuwa na mahitaji maalumu.Viashiria hivi vinaweza kuwa ni hali yoyote ya kuchelewa hatua za ukuaji, maumbile,  matendo na tabia yasiyokuwa ya kawaida kulingana na matarajio ya ukuaji. Shughuli ya ubainishaji inaweza kufanyika wakati wowote baada ya mtoto kuzaliwa au akiwa shuleni. Aidha, ubainishaji unafanywa na mtu yeyote wakiwemo wazazi, wanafamilia, wataalamu mbalimbali na jamii kwa ujumla.

## 2.3 Maeneo yanayotumika katika Ubainishaji na Utambuzi wa awali

Ubainishaji na utambuzi wa awali wa mahitaji ya kielimu ya watoto wenye mahitaji maalumu yanaweza kufanywa katika mazingira ambamo mtoto anapatikana. Mazingira hayo yanaweza kuwa nyumbani, shuleni au katika mazingira yake ya kucheza.

## 2.4 Viashiria

Mahitaji maalumu ya mtoto yanaweza kubainishwa kwa kuangalia viashiria mbalimbali kulingana na changamoto aliyonayo. Baadhi ya

viashiria hivyo ni kama vilivyoainishwa hapa chini:

### 2.4.1 Changamoto za uoni

i. Macho kuchezacheza kusiko kwa kawaida
ii. Mwonekano wa jicho usio wa kawaida (mfano makengeza)
iii. Kujigonga mara kwa mara kwenye vitu wakati wa kutembea
iv. Kuongozwa wakati wa kutembea
v. Kutembea kwa woga na kutojiamini
vi. Kufikicha macho
vii. Kutokwa na machozi mara kwa mara
viii. Kushindwa kutofautisha rangi
ix. Malalamiko ya kichwa au macho kuuma mara kwa mara
x. Kusogea karibu sana na kitu ili kukiona
xi. Kukaza sana macho wakati wa kusoma au kuangalia kitu hasa chenye umbo dogo

**Zana zinazoweza kutumika katika kubaini**

i. Chati za picha
ii. Mwanasesere
iii. Vifani
iv. Vitu vyenye unamu tofauti
v. Vitu vyenye rangi mbalimbali

### 2.4.2 Changamoto za usikivu

i. Kutoitika au kuchelewa kuitika
ii. Muonekano wa umbo la sikio/masikio usio wa kawaida
iii. Kutokwa na usaha sikioni au masikioni
iv. Kuongea kwa sauti kubwa kuliko au ndogo
v. Kushindwa kutofautisha sauti mbali mbali
vi. Kutembea kwa kuburuza miguu na kukosa msawazo wa mwili
vii. Kuelekeza sikio la upande mmoja kwenye chanzo cha sauti
viii. Kuangalia midomo ya mtu anayeongea
ix. Kutotambua chanzo na mwelekeo wa sauti
x. Wakati wote hujieleza kwa ishara badala ya sauti
xi. Kujitenga na wanarika wenzake kwa sababu ya kushindwa kuwasiliana

**Zana zinazoweza kutumika katika kubaini**

i. Ngoma
ii. Manyanga
iii. Kengele ndogo
iv. Filimbi
v. Vifaa vinavyoweza kutoa sauti
vi. Kupiga makofi, kuimba au kuita

### 2.4.3 Changamoto za Uziwi/Kutoona

i. Mwonekano wa jicho/macho usio wa kawaida
ii. Kujigonga mara kwa mara kwenye vitu wakati wa kutembea
iii. Kuongozwa wakati wa kutembea
iv. Malalamiko ya macho na/au masikio kuuma mara kwa mara
v. Kutokwa na usaha sikioni au masikioni
vi. Kusogea karibu sana na kitu ili kukiona
vii. Kutoitika au kuchelewa kuitika
viii. Kutembea kwa kuburuza miguu na kukosa msawazo wa mwili
ix. Kujieleza kwa ishara badala ya sauti
x. Kujitenga
xi. Kutumia zaidi mlango baki wa kunusa na kugusa

**Zana zinazoweza kutumika katika kubaini**

i. Chati za picha zenye rangi tofauti
ii. Vifani vyenye unamu tofauti
iii. Vitu vyenye rangi za kung'aa
iv. Vitu vinavyotoa sauti tofauti

### 2.4.4 Changamoto za ufahamu

i. Kutopenda kuangaliana uso kwa uso
ii. Kuwa jasiri pasipo woga
iii. Tabia ya kuharibu vitu
iv. Kupenda kujitenga
v. Kuunguruma,kupiga kelele, kucheka au kulia nje ya muktadha
vi. Kujidhuru au kudhuru watu wengine
vii. Tabia ya kupenda kurudiarudia matendo au kufanya jambo moja kwa muda mrefu
viii. Kupenda kunusanusa
ix. Muonekano kimaumbile, mfano kuwa na kichwa kikubwa au kidogo kupita kiasi na sura ya mduara yenye macho madogo yasiyowiana na ukubwa wa kichwa
x. Kutokwa na udenda
xi. Utulivu au utundu kupita kiasi
xii. Kushindwa kuongea na kujieleza (tatizo la mawasiliano), kufuata maelekezo, kumudu mazingira
xiii. Kushindwa, kupambanua, kulinganisha na kupanga vitu kwa utaratibu

xiv. Kuwa na uwezo mdogo katika stadi za kujimudu kwa umri stahiki
xv. Tabia za kudakia na kuingilia jambo kabla ya wakati wake
xvi. Wepesi wa kuelewa dhana mpya na msamiati wakati wa ujifunzaji
xvii. Kukosa utulivu kutokana na kazi zisizowavutia
xviii. Kushindwa kumudu stadi za kujieleza, kusoma, kuandika, kuhesabu na kutafsiri
xix. Kukata tamaa katika ujifunzaji

**Zana zinazoweza kutumika katika kubaini**

i. Vibao jenga
ii. Chati za picha za ukutani
iii. Mipira ya ukubwa na rangi tofauti
iv. Shanga zenye ukubwa tofauti na rangi mbalimbali
v. Mwanasesere

### 2.4.5 Changamoto ya Ualbino

Muonekano wa ngozi, nywele au macho tofauti na inavyotarajiwa

### 2.4.6 Changamoto za kiafya

i. Muonekano wa mwili/udhaifu/ngozi isiyo na afya
ii. Kuwa mnyonge muda wote
iii. Kukohoa kusiko kwa kawaida
iv. Malalamiko ya kuugua mara kwa mara

### 2.4.7 Changamoto za kijamii

i Kuwa wanyonge na kutochangamka
ii Kukosa mahitaji muhimu ya ki-utu

### 2.4.8 Changamoto za ujongeaji

i Kutokuwa na kiungo fulani katika mwili wake
ii Kuwa na viungo dhaifu/kushindwa kukaa/kusimama/kutembea
iii Viungo vya mwili kuwa na umbo lisilo la kawaida.

**Zana zinazoweza kutumika katika kubaini**

i. Vifaa mbalimbali vya kuchezea
ii. Mwanasesere

iii. Matendo ya mwili (kutembea, kukaa, kukimbia, kusimama, kula)

## 2.5 Umuhimu wa Ubainishaji na Utambuzi

i. Mzazi/ mlezi kupata maelekezo ya kumpeleka mtoto kwa wakati katika kituo cha upimaji kwa uchunguzi zaidi
ii. Watoto watapata afua stahiki kwa wakati hivyo kuzuia au kuondoa changamoto aliyonayo mtoto
iii. Serikali kuweza kupata maoteo (*projection*) ya watoto wenye mahitaji maalumu watakaoandikishwa darasa la awali na darasa la kwanza.
iv. Wanafunzi walioko shuleni watakaobainika kuwa na mahitaji maalumu watapata afua kulingana changamoto iliyobainika.

Baada ya mtoto kubainika kuwa na viashiria vya mahitaji maalumu, mzazi/mlezi ashauriwe kumpeleka mtoto katika kituo cha upimaji kwa ajili ya kufanyiwa upimaji na ushauri.

## 2.6 Utekelezaji wa shughuli ya ubainishaji na utambuzi wa awali

### 2.6.1 Halmashauri

Utekelezaji wa shughuli za ubainishaji na utambuzi katika halmashauri zitakuwa chini ya Mkurugenzi kupitia idara zinazohusika na huduma kwa watu wenye mahitaji maalumu kama inavyobaishwa hapo chini. Pia, halmashauri inatakiwa kuhakikisha jamii inajengewa uwezo wa kubaini na kutambua viashiria vya mahitaji maalumu kwa watoto. Hii itasaidia jamii kuweza kubaini watoto wenye wenye mahitaji maalumu kwenye familia zao na jamii kwa ujumla.

**i. Idara ya Elimu**

a. Kuandaa mpangokazi wa utekelezaji wa zoezi la ubainishaji na utambuzi
b. Kusimamia uendeshaji wa zoezi la ubainishaji na utambuzi
c. Kuandaa, kutunza na kutumia kanzidata ya watoto wanaobainika kuwa na mahitaji maalumu
d. Kufuatilia utekelezaji wa ushauri uliotolewa kwa watoto waliobainishwa

**ii. Idara ya Afya**

a. Kubaini watoto wenye changamoto za kiafya
b. Kutoa ushauri wa namna ya kutunza afya kwa watoto, wazazi/walezi wanaofika kubainishwa
c. Kuweka utaratibu wa kutoa huduma stahiki kwa watoto

wanaopewa rufaa kutoka vituo vya upimaji kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa

d. Kuhamasisha jamii kushiriki katika zoezi la ubainishaji na utambuzi
e. Kushirikiana na timu ya ubainishaji na upimaji

### 2.6.2 Wabainishaji

Katika utekelezaji wa majukumu yake, mbainishaji atamtambua mtoto mwenye mahitaji maalumu kwa kutembelea jamii baada ya kupata kibali kutoka katika mamlaka ya Serikali katika eneo alilopangiwa kufanya ubainishaji na utambuzi.

Aidha mbainishaji akitambua uwepo wa viashiria vya mahitaji maalumu, atajaza fomu rasmi ya ubainishaji na kumpatia mzazi/mlezi ili iweze kumsaidia kufikisha taarifa za mtoto kwenye kituo cha upimaji. Ikiwa ni mzazi/mlezi ndiye aliyebaini, anaweza kumpeleka mtoto moja kwa moja kwenye kituo cha upimaji au kutoa taarifa kwenye mamlaka zinazohusika kwa hatua zaidi.

### 2.6.3 Hitimisho

Utambuzi ni hatua ya awali na muhimu katika kuhakikisha mtoto mwenye mahitaji maalumu anatambuliwa na kupewa afua stahiki. Zoezi hili ni lazima lifanywe kwa umakini na kwa kuzingatia unyeti wa mahitaji maalumu. Aidha, mbainishaji hana budi kutambua tamaduni za jamii husika ili kuhakikisha hasababishi migogoro katika jamii/familia. Ni muhimu kwa mbainishaji kusoma na kuelewa viashiria ili aweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

SURA YA TATU

# UPIMAJI WA KUBAINI MAHITAJI YA UJIFUNZAJI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza uanzishwaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji kwa kuangalia dhana ya upimaji, muundo wa timu ya upimaji, sifa na usimamizi wa vituo vya upimaji. Pia inaainisha majukumu ya timu ya upimaji na kanuni za uendeshaji wa vituo vya upimaji.

## 3.2 Dhana ya upimaji

Upimaji wa mahitaji maalumu ya ujifunzaji ni mchakato wa ukusanyaji wa taarifa juu ya uwezo na changamoto alizonazo mtoto ili kuweza kubaini mahitaji yake kwa lengo la kutoa afua stahiki.

## 3.3 Timu ya upimaji

Kutakuwa na timu ya upimaji wa mahitaji ya ujifunzaji kwa kila halmashauri itakayoratibiwa na Afisa Elimu-Elimu Maalumu. Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kuunda na kusimamia timu hii. Pia, Mkurugenzi anatakiwa kuweka utaratibu wa mafunzo endelevu kwa wataalamu wanaounda timu ya upimaji. Timu ya upimaji itakuwa na wataalamu wasiopungua watano kama ilivyoainishwa hapa chini:

i. Walimu wa elimu maalumu wasiopungua watatu kutoka katika fani tofauti. Mfano:
   a. Uziwi
   b. Wasioona
   c. Ulemavu wa akili na usonji
   d. Uziwikutoona
ii. Wataalamu wawili kutoka idara ya afya
   a. Daktari au Muuguzi
   b. Afisa ustawi wa jamii

**Muhimu**

**1**. Wataalamu wengine kama vile wanasaikolojia, mtaalamu wa tiba viungo au mtaalamu wa matamshi wanaweza kuhusiswa katika timu kulingana na mahitaji.

**2.** Wataalamu watakaochaguliwa wapewe angalau siku mbili kila wiki ili waweze kutoa huduma za upimaji kituoni.

Timu itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kuendesha shughuli za upimaji wa watoto ili kutambua uwezo na mahitaji ya ujifunzaji
ii. Kushauri na kutoa afua stahiki ikiwa ni pamoja na rufaa ya mtoto kwa lengo la kupata msaada zaidi
iii. Kufanya ufatiliaji wa maendeleo ya mtoto kwenye maeneo anayopatiwa huduma ikiwa ni pamoja na kushirikiana na walimu kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa mpango binafsi wa kielimu (*Individualized Education Program [IEP])*
iv. Kutunza takwimu na taarifa za watoto wenye mahitaji maalumu waliohudumiwa kituoni
v. Kuandaa taarifa ya mwezi juu ya utekelezaji wa kazi zilizofanyika kwenye kituo cha upimaji

### 3.4 Uanzishaji na usimamizi wa vituo vya upimaji

Kila Hamshauri inaelekezwa kuanzisha na kuendesha kituo cha upimaji kwa lengo la kuainisha mahitaji maalumu ya ujifunzaji kwa mtoto ili kupatiwa afua stahiki. Kituo kitaendeshwa na timu ya wataalamu wa upimaji chini ya Mkurugenzi wa halmashauri kama ilivyohainishwa kwenye kipengere 3.3 cha Mwongozo huu.
Kituo cha upimaji kinatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:
i. Kiwe kwenye eneo ambalo linafikika kwa urahisi na lenye mazingira rafiki
ii. Kituo kiwe na jengo lenye vyumba visivyopungua vitatu, ambapo chumba kimojawapo kiwe ni kile kisichoruhusu sauti kupenya kwa ajili ya upimaji wa usikivu (*soundproof room)*
iii. Kituo kiwe na samani zote za muhimu kwa ajili ya ofisi na wageni
iv. Kituo kiwe na vifaa mbalimbali vya upimaji kama vile:
    a. Vifaa vya kupima usikivu
    b. Vifaa vya kupima uoni
    c. Vifaa vya kupima ufahamu
    d. Vifaa vya kupima namna ya mawasiliano
v. Kituo kiwe na vifaa vya uendeshaji wa ofisi kama vile kompyuta, karatasi na mashine ya kudurufu
vi. Kituo kiwe na vyombo vya usafiri vitakavyowawezesha wataalamu wa upimaji kufika kwenye maeneo mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye kipengele 3.3 katika Mwongozo huu

### 3.5 Kanuni za uendeshaji wa vituo vya upimaji

Ili kuleta ufanisi katika kazi ya upimaji, kanuni zifuatazo zizingatiwe:
i. Kutunza kwa usiri taarifa za wazazi na watoto wanaopimwa

kituoni

ii. Kuwa mvumilivu na kutumia lugha yenye staha
iii. Kuzingatia sera, sheria na miongozo kuhusu huduma kwa mtoto nchini Tanzania
iv. Kufuata taratibu, kanuni na sheria za utumishi wa umma wa Tanzania

### 3.6 Hitimisho

Ni muhimu kwa timu ya upimaji kutambua kwamba mchakato wa upimaji unahusisha uainishaji wa uwezo na changamoto za mtoto na kutafsiri matokeo ya upimaji na kutoa mrejesho. Pia upimaji unahusisha uwekaji wa mikakati na utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini.

SURA YA NNE

# USHIRIKI WA WADAU KATIKA UBAINISHAJI, UTAMBUZI NA UPIMAJI

## 4.1 Utangulizi

Zoezi la ubainishaji, uambuzi, na upimaji linaweza kufanyika kwa ufanisi mkubwa endapo litashirikisha wadau mbalimbali. Sura hii inafafanua ushiriki wa wadau hao katika zoezi hilo kwa kuainisha makundi ya wadau na majukumu yao.

## 4.2 Makundi ya wadau

Wadau ni watu, jamii, makundi au taasisi zinazojihusisha na utekelezaji wa mchakato wa ubainishaji, utambuzi na upimaji wa mahitaji ya ujifunzaji. Baadhi ya makundi haya ni kama ifuatavyo:

i. Vyama vya watu wenye ulemavu
ii. Asasi zinazohudumia watu wenye mahitaji maalumu
iii. Vyuo vinavyohudumia watu wenye mahitaji maalumu
iv. Taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa zinazohudumia watu wenye mahitaji maalumu
v. Wazazi
vi. Jamii
vii. Watu binafsi

### 4.2.1 Majukumu ya vyama vya watu wenye ulemavu

Vyama vya watu wenye ulemavu vitakuwa na majukumu ya kufanya uhamasishaji wa jamii juu ya umuhimu wa kuwabainisha na kuwatambua watu wenye ulemavu.

### 4.2.2 Asasi zinazohudumia watu wenye mahitaji maalum

Majukumu ya ASASI zinazohudumia watu wenye mahitaji maalumu ni pamoja na kutoa ufadhili wakati wa mchakato wa ubainishaji na utambuzi.

### 4.2.3 Vyuo vinavyohudumia watu wenye mahitaji maalumu

Vyuo vinavyohudumia watu wenye mahitaji maalumu watakuwa na jukumu kuandaa na kuwasilisha tafiti mbalimbali zinazowezesha upatikananji wa taarifa ya hali halisi ya maeneo ambayo kuna idadi ndogo au kubwa ya watoto wenye mahitaji maalumu na aina ya

mahitaji yanayotakiwa. Aidha, vyuo vinaweza kushiriki katika kuwezesha mafunzo ya ubainishaji.

### 4.3 Hitimisho

Watoto wenye mahitaji maalumu wamekuwa wakipitia katika changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kukosa haki ya elimu. Hii imetokana na ukweli kwamba jamii imekuwa na kasumba ya kuwaficha watoto hao hali inayosababisha kuchelewa kubaishwa kwa ajili ya kutambuliwa na kupewa afua stahiki. Ushiriki wa jamii na wadau mbalimbali kwenye jukumu la ubainishaji na utambuzi utaisaidia Serikali katika kutimiza azma yake ya kuwahudumia watoto husika. Kama ilivyoainishwa katika Sura hii, kila mdau ana jukumu la kutekeleza katika kuhakikisha tunajenga jamii yenye haki na usawa.

SURA YA TANO

# UKUSANYAJI, UTUNZAJI NA UTUMIAJI WA TAARIFA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha fomu zinazotumika katika ukusanyaji wa taarifa zinazotokana na matokeo ya utambuzi, ubainishaji na upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu. Pia inaelekeza namna ya utunzaji na utumiaji wa taarifa zinazotokana na upimaji. Mtumiaji wa Mwongozo huu anapaswa kuhakikisha fomu zilizoainishwa katika Sura hii zinatumika ipasavyo ili kuleta ufanisi uliokusudiwa.

## 5.2 Ukusanyaji wa taarifa za upimaji

Kwa kuzingatia malengo ya Mwongozo huu, ukusanyaji wa taarifa utafanywa kwa kutumia fomu zifuatazo:

i. Fomu ya utambuzi (*tazama Kiambatisho A*)
ii. Fomu ya mpango wa tarehe ya upimaji (*tazama Kiambatisho B*)
iii. Fomu ya upimaji (*tazama Kiambatisho C*)
iv. Fomu ya matokeo ya upimaji (*tazama Kiambatisho D2*)
v. Fomu ya rufaa (*tazama Kiambatisho D3*)

## 5.3 Utunzaji wa taarifa za upimaji

Kumekuwa na tabia za kutumia vibaya taarifa za mtoto zinazotokana na ubainishaji. Tabia hizi zinajumuisha upigaji na utumiaji wa picha bila ridhaa ya mhusika. Hii ni kinyume cha sheria na ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Sehemu hii inasisitiza umuhimu wa utunzaji wa siri kwa kuzingatia sheria ya mtoto ya mwaka (2009) inayosisitiza haki, ulinzi na usalama wa mtoto. Vile vile kwa kuzingatia Mwongozo wa malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto kwa shule na vyuo vya ualimu Tanzania (2020) na miongozo mingine iliyowekwa na serikali.

## 5.4 Utumiaji wa taarifa za upimaji

Sambamba na ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za ubanishaji, sehemu hii inaelekeza kwamba taarifa zilizotokana na upimaji zitumike kwa ajili ya kupendekeza eneo stahiki la kupatiwa huduma kulingana na mahitaji ya mtoto mwenye mahitaji maalumu; shuleni, hospitali au vituo vya huduma za utengamao. Hivyo taarifa za mtoto zitumike tu kwa malengo yaliyokusudiwa. Itakuwa ni ukiukwaji haki za binadamu na uvunjaji wa sheria za nchi kutumia taarifa za mtoto kinyume na malengo tarajiwa. Mtekelezaji wa Mwongozo huu anawajibika kuhakikisha kuwa taarifa yoyote inayotokana na ubainishaji, utambuzi na upimaji inabaki kuwa

siri na inalindwa na Sheria ya Takwimu Na. 9 ya mwaka 2015.

### 5.5 Hitimisho

Kwa miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na kupishana kwa taarifa zinazohusiana na wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hii imesabisha kutopata taarifa sahihi na hivyo kufifisha malengo ya kuweka mipango ya huduma za kielimu kulingana na idadi halisi ya wanafunzi. Utumiaji wa Mwongozo huu utasaidia kuwa na takwimu sahihi za watoto wenye mahitaji maalumu katika eneo husika ili kuandaa mipango ya utoaji wa huduma stahiki.

SURA YA SITA

# MAJUMUISHO

## 6.1 Utangulizi

Sura hiii inatoa muhtasari wa mada zilizowasilishwa katika Mwongozo huu kwa kuangazia baadhi ya mambo muhimu ambayo mtekelezaji wa Mwongozo anatakiwa kuyazingatia ili kuleta ufanisi. Hivyo, sura imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni utangulizi, majumuisho na hitimisho.

## 6.2 Majumuisho

Serikali na wadau mbalimbali wamekua wakishilikiana katika kufanya kazi zaubainishaji, utambuzi na upimaji kwa watoto ili kubaini mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki. Katika kutekeleza majukumu yake, OR-TAMISEMI imebaini kwamba kuna umuhimu wa kuanzishwa kwa vituo vya upimaji kwa ngazi ya halmashauri ili kusogeza kwa walengwa. Hivyo, Mwongozo huu unatoa maelekezo yanayopaswa kutekelezwa na halmashauri katika kuanzisha na kuendesha vituo hivyo. Hivyo, kila ngazi ya halmashauri iliyotajwa katika Mwongozo huu inajukumu la kuusoma na kuuelewa kwa kina ili kutekeleza maelekezo yaliyotolewa. Hii itasaidia kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa afua stahiki.

## 6.3 Hitimisho

Serikali imekuwa ikifanya shughuli ya ubanishaji ili kutambua watoto wenye mahitaji maalumu kwa lengo la kuwapatia afua stahiki ikiwa ni pamoja na elimu. Moja ya changamoto ziliyobainika katika mchakato huo ni kwa watoto waliobainishwa kupelekwa shuleni pasipo kupitia vituo vya upimaji kutokana na uhaba wa vituo vya upimaji. Hivyo, kwa kuzingatia nia ya serikali ya kutoa elimu bora kwa wote pamoja na watoto wenye mahitaji maalumu, serikali imeelekeza kuanzishwa kwa vituo vya upimaji katika ngazi ya halmshauri. Hii itasaidia watoto wenye mahitaji maalumu kubainishwa mapema na kupewa afua stahiki kabla na/au baada ya kuandikishwa shule.

# REJEA

IDPC. (2016). *Kamusi Elekezi ya Ulemavu: Kingereza – Kiswahili*. Dar es Salaam- Tanzania

JMT. (2013). *Mwongozo wa Utambuzi wa Mapema wa Watoto Wenye Mahitaji Maalumu na Afua Stahiki Umri (miaka 0-18)*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

JMT. (2013). *Rasimu ya Mwongozo Elekezi wa Kubaini Mahitaji Maalumu: Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa Watoto*.Dar es Salaamu: WyEST

JMT. (2021). *Mwongozo wa Taifa wa Utambuzi wa Mapema na Afua Stahiki kwa Watoto Wenye Ulemavu*. Dodoma: Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu. Dodoma: Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu

URT (2013). *Guidelines for Educational Support, Resource and Assessment services*. Dar es Salaam: MoEVT & UNICEF

URT (2014). Operational Tools for Effective Management of ESRAC. Dar es Salaam: MoEVT & IAS

URT (2021). National Strategy for Inclusive Education 2021/22-25/2026. Dodoma: MoEST

*Kiambatisho A*

## FOMU YA UTAMBUZI

KITUO CHA UPIMAJ I...........................................................................................................
JINA LA MTOTO ..............................................................................................................
TAREHE YA KUZALIWA .................................... UMRI ........... JINSI..............................
SHULE/KIJIJI/MTAA...........................................................................................................

## VIASHIRIA VILIYOBAINIKA

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

Ninamleta kwako mtajwa hapo juu kwa upimaji/uchunguzi/ ushauri kwa hatua zaidi.

## FOMU YA MPANGO WA TAREHE YA UPIMAJI

**TAREHE YA KWENDA KITUONI KWA AJILI YA UPIMAJI ..................................**

| NO | JINA LA MTOTO | NAMBA YA SIMU | MAHALI ANAKOISHI |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**FOMU YA UPIMAJI**

JINA LA KITUO CHA UPIMAJI ..........................................................................................

**SEHEMU YA I:**

(Ijazwe na wapimaji tu)

**TAARIFA ZA MTOTO**

Jina ........................................................................................................................................

Jina alilozoea mtoto ................................................................................................................

Jinsi:............................... tarehe ya kuzaliwa .............................umri .........................

Shule.........................................Anwani..................................................................................

Urefu..................................................Uzito.............................................................................

Jina la baba .........................................umri..........................................................................

Kazi..........................................................................................................................................

Anwani ya kudumu: ............................................. simu ...............................................

Jina la mama .................................... Umri ..........................................................................

Kazi..........................................................................................................................................

Anwani ya kudumu....................................Simu ..........................................................

Mlezi ............................Simu......................................................................................

Kazi..........................................................................................................................................

Anwani ya kudumu.................................................................................................................

Halmashauri ya Wilaya ........................................Kata..................................................

Kijiji/Mtaa..............................................................................................................................

Namba ya nyumba..................................................................................................................

Kabila..................................Uraia.........................................................................................

Mahali alikozaliwa.................................................................................................................

Lugha inayotumika nyumbani.............................................................................................

Idadi ya watoto waliozaliwa tumbo moja ..........................................................

Wa ngapi kuzaliwa: .................. Walio hai.......................................................................

Kuna mwenye ulemavu wa aina yoyote katika famila/ukoo?

Ndiyo......................................................................................................................

Hapana...................................................................................................................

Kama ndiyo, toa maelezo ..........................................................................................................................

..........................................................................................................................................................................

**HISTORIA KABLA NA WAKATI WA KUZALIWA.**
Mtoto alizaliwa nyumbani/kituo cha afya/hospital / hospitali ya rufaa?Mama alipatwa na tatizo lolote wakati wa ujauzito? ..............................................................................................................................................

mfano magonjwa ya zinaa, Malaria, Uti wa mgongo,kifafa cha mimba
Ikiwa jibu ni ndiyo, tafadhali fafanua: ...............................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................

Je, mama alipata changamoto yoyote wakati wa kujifungua? ..................................................................
..............................................................................................................................................................

Ikiwa jibu ni ndiyo, tafadhali fafanua: ...............................................................................................................
...............................................................................................................................................................

Je, mtoto alizaliwa kabla ya wakati wake?.............................................................................................
Kama jibu ni ndiyo, ni kwa muda/miezi mingapi?.................................................................................
Je, uchungu wa uzazi ulikuwa kwa muda gani?.....................................................................................
Je, mtoto alilia/ kutoa sauti mara baada ya kuzaliwa?.........................................................................

**HISTORIA YA MTOTO**:
Je, mtoto alipata kuugua homa yoyote baada ya kuzaliwa?.................................................................
Je, mtoto ana Changamoto yoyote kwa sasa?
Ikiwa jibu ni ndiyo, tafadhali fafanua
.........................................................................................................................................................................
.........................................................................................................................................................................

Ni kwa muda gani mtoto alianza:
Kukaa.............................................................
Kusimama..................................................
Kutembea...................................................
Kuongea......................................................

Ni kwa jinsi gani mtoto anajieleza ikiwa anahitaji msaada wowote?
.........................................................................................................................................................................
.........................................................................................................................................................................

Je, mtoto anahitaji msaada wowote kwenda chooni? (asubuhi/mchana/usiku/wakati wowote .
.........................................................................................................................................................................
.........................................................................................................................................................................
.........................................................................................................................................................................

Nini changamoto katika huduma za kujimudu?.
...........................................................................................................................................
...........................................................................................................................................
...........................................................................................................................................

## TATHMINI YA UTENDAJI

| NA. | ENEO | JINSI YA UPIMAJI | MATOKEO |
|---|---|---|---|
| 1 | UFAHAMU | • Kupanga vibao ili kupima utendaji wa macho na misuli ya mikono<br>• Vifaa cheza (puzzles) kwa ajili ya kupima ufahamu<br>• Mipira kwa lengo la kupima ufahamu wa dhana ya ukubwa, uzito, urefu, ufupi<br>• Michezo ya kupima uwezo wa kutunza kumbukumbu, kufanya maamuzi,kutofautisha rangi<br>• Kupima uwezo wa kusoma na kuandika kwa awali (kusema neno, kuhusianisha neno/ maneno na herufi)<br>• Kuonesha sehemu za mwili | |
| 2 | UTENDAJI WA MISULI MIDOGO | • Kushika na kuachia vitu<br>• Kuchora na kupaka rangi<br>• Kunakili umbo/herufi/maandishi<br>• Kuandika kwa kuchorachora (hata kama sio kwa uzuri/umbo linaloeleweka) | |
| 3 | UTENDAJI WA MISULI MIKUB-WA | • Kupiga mpira<br>• Kurusha na kudaka mpira<br>• Kusimama kwa mguu mmoja<br>• Kuruka au kukimbia | |
| 4 | LUGHA NA MAWASILIANO | • Kujieleza: Ikiwa anaweza;<br>i. kusema sentensi fupi,<br>ii. kutamka vyema maneno/sentensi,<br>iii. kurudia kuyatamka maneno baada ya mwingine.<br>• Upokeaji wa taarifa:<br>i. kuitikia/ kufuata maelekezo anayopewa,<br>ii. kutambua picha,<br>iii. kufuata maelekezo ya tendo la; kulia, kushoto, katikati, mbele au nyuma (Mpimaji aangalie jinsi ya utamkaji, kigugumizi au mkwamo wa sauti) | |
| 5 | TABIA/ MWENENDO | Angalia maeneo yafuatayo, au zaidi ya;<br>• utundu/kutokutulia<br>• upole kupita kiasi<br>• utulivu wa kusikiliza<br>• udadisi<br>• kujiondoa kwenye mazungumzo/ushiriki wa jambo<br>• kuuma meno kwa mfululizo<br>• kujitenga | |
| 6 | UONI NA UJO-NGEAJI | • Uoni wa kutosha<br>• Angalia mjongeo (mf. Kupanda ngazi, kutembea...)<br>• Macho yanayotoa machozi<br>• Kusogeza kitabu karibu na macho wakati wa kusoma | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | USIKIVU | • Jinsi anavyotamka<br>• Jinsi anavyoelekeza sikio kuelekea upande wa sauti<br>• Kutoa sauti kubwa au ndogo zaidi ya kiwango tarajiwa<br>• Kuchoka mapema katika kuzungumza<br>• Kukosa uvumilivu<br>• Kutumia ishara au lugha ya alama<br>• Ikiwa anazungumza huku akitazama midomo au mzungumzaji<br>• Kushindwa kutofautisha sauti mbalimbali<br>• Kutembea kwa kuburuza miguu ardhini | |
| 8 | VIUNGO | • Mjongeo wa misuli usio wa kawaida<br>• Mkakamao<br>• Kukosa viungo<br>• Kukosa msawazo wa mwili<br>• Kupooza kwa mwili (upande mmoja au zaidi) | |
| 9 | USONJI | Chunguza yafuatayo, au zaidi;<br>• Tabia za kujirudiarudia<br>• Kujitenga<br>• Changamoto za mawasiliano<br>• Kunusa vitu, vyakula au watu<br>• Kutoa sauti zisizo za kawaida/kwa kurudiarudia<br>• Uwezo wa kufuata maelekezo/kuelewa (hata kama ni madogo)<br>• Uwezo wa kuhusianisha vitu | |
| 10 | CHANGAMOTO ZA UJIFUNZAJI | Angalia maeneo yafuatayo, au zaidi ya;<br>i. Kushindwa;<br>a) kusoma (Dyslexia)<br>b) kuhesabu (Dyscalculia)<br>c) kuzungumza (Aphasia)<br>d) kuandika (Dysgraphia)<br>ii. Kushindwa kufuata maelekezo ukilinganisha na watoto wengine wa umri wake<br>iii. Kushindwa kufuata maelekezo ya mfululizo/ mfuatano<br>iv. Kupendelea michezo zaidi | |

**MATOKEO YA JUMLA**

Uwezo uliobainika

...........................................................................................................
...........................................................................................................
...........................................................................................................

Udhaifu uliobainika

...........................................................................................................
...........................................................................................................
...........................................................................................................

Mpango wa kielimu unaopendekezwa

...........................................................................................................
...........................................................................................................
...........................................................................................................

Malengo ya muda mfupi

...........................................................................................................
...........................................................................................................
...........................................................................................................

Malengo ya muda mrefu

...........................................................................................................
...........................................................................................................
...........................................................................................................

A. Mapendekezo

-..........................................................................................................
...........................................................................................................

B. Maoni

...........................................................................................................
...........................................................................................................
...........................................................................................................

**Taarifa hii imetolewa na:**

.......................................................................................................................
Jina.........................Cheo cha kazi.....................................................
Saini........................................Tarehe.........................................................

Jina la Mtaalamu/Mpimaji..........................................................................
Jina la kituo cha Upimaji.........................................................................
Saini.......................................Tarehe...................................................................

**FOMU YA RUFAA**

KWENDA KWA.................................................................................................
MKOA................................................WILAYA..................................................
KITUO CHA UPIMAJI....................................................................................
JINSI...............................................................................
TAREHE KUZALIWA..............................................UMRI..........................
JINA LA BABA.................................................SIMU...............................
JINA LA MAMA.................................................SIMU...............................
JINA LA MLEZI.................................................SIMU...............................

UCHUNGUZI WA KITABIBU

.....................................................................................................................

MATOKEO YA UPIMAJI WA MAHITAJI YA KIELIMU

.....................................................................................................................
.....................................................................................................................
.....................................................................................................................
.....................................................................................................................

UWEZO ULIOBAINIKA/ALIONAO

.....................................................................................................................
.....................................................................................................................
.....................................................................................................................
.....................................................................................................................

UDHAIFU ULIOBAINIKA/ALIONAO

.....................................................................................................................
.....................................................................................................................
.....................................................................................................................

RUFAA HII NI MAALUMU KWA AJILI YA KUANDAA MPANGO WA KIELIMU

...................................................................................................................
...................................................................................................................
...................................................................................................................
...................................................................................................................
...................................................................................................................
...................................................................................................................
...................................................................................................................
...................................................................................................................

Majina ya wataalamu wa upimaji

1. .......................................Saini..................................Tarehe............................
2. .......................................Saini..................................Tarehe............................
3. .......................................Saini..................................Tarehe............................
4. .......................................Saini.................................. Tarehe............................

**Mji wa Magufuli - Mtumba**
Mtaa wa TAMISEMI
S.L.P 1923,
41185 Dodoma, Tanzania
**Simu** : (255) 26 232 1 234
**Barua Pepe** : ps@tamisemi.go.tz

**www.tamisemi.go.tz**